


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA



National Arts Council

Tarehe: 14/02/2017

TANGAZO KWA WASANII NA WADAU WOTE WA SANAA

YAH: WASANII KUJITOLEA KUPOKEA KIFIMBO CHA MALKIA WA UINGEREZA

Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) linawataarifu kuwa limepokea taarifa kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo juu ya kuwasili kwa kifimbo cha Malkia wa Uingereza (Queen's Button) kinachotarajiwa kuwasili nchini tarehe 08/04/2017 na kitapokelewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano Mhe. John Pombe Magufuli tarehe 09/04/2017.

Baraza linawahimiza wasanii wote kujitolea kutoa burudani bila malipo sehemu mbalimbali wakati wa mapokezi hayo. Baraza linaona kuwa hii itakuwa fursa kwa wasanii kujitangaza katika soko la kimataifa kwani ziara ya kifimbo cha Malkia hufuatiliwa na Mitambo ya Satellite ambapo tukio hili litaonekana dunia nzima.

Wasanii ambao watakuwa tayari kujitolea kutoa burudani tafadhali Baraza linaomba kupata majina yao kabla ya tarehe 22/02/2017.

Kwa maelezo zaidi, unaweza kufika Baraza la Sanaa la Taifa, Ilala Shariff Shamba, Dar es salaam au piga simu namba. 2863748

Nakutakia maandalizi mema.

Godfrey L. Mngereza
KATIBU MTENDAJI

Barua zote ziandikwe kwa Katibu Mtendaji

All correspondence to be addressed to The Executive Secretary

BASATA Arts Centre, Ilala Sharif Shamba, P.O. Box. 4779, Dar es Salaam, Tanzania.

Telephone: 2863748/2860485, Fax: 0255 - (022) - 286 0486 E-mail: info@basata.or.tz Website: basata.go.tz